



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Unapojibu tafadhali taja:

KUMB. NA. AC/18/214/65

Tarehe : 16/08/2023

TANGAZO LA NAFASI 29 ZA KUKUSANYA MAPATO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE .

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anawatangazia Wananchi wa Wilaya ya Nyang'hwale nafasi za kazi.

Hivyo, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.

WANAOHITAJIKA

- ❖ Wakusanya mapato nafasi (29)

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kukusanya mapato katika eneo utakalopangiwa na Mwajiri
- ii. Kuhakikisha mapato yote ya Halmashauri yanakusanywa kwa kufuata taratibu
- iii. Kupeleka Benki fedha yote inayokusanywa kwa wakati

SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe ni Mwananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale (Mkazi)
- ii. Mwombaji awe anajua kutumia simu janja (Smart phone)
- iii. Awe na Kitambulisho cha NIDA
- iv. Awe na afya njema, mwaminifu, mwenye kujituma
- v. Awe muhitimu kidato cha nne

vi. Mwombaji awe ni Mtanzania asiyezidi umri wa miaka 45, awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

vii. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma

viii. Mwombaji awe mkazi wa kijiji husika na barua zote za maombi zipitie kwa Mtendaji wa kijiji.

ix. Mwombaji awe na mdhamini mwenye mali isiyohamishika na awe mkazi wa eneo husika..


x. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **25/08/2023 saa 9:30 alasiri**. Aidha maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S. L.P 352

NYANG'HWALE.

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri www.nyang'hwaledc.go.tz na katika mbao za matangazo.


Majagi R. Maiga
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NYANG'HWALE.

MKURUGENZI MTENDAJI
S.L.P 352
NYANG'HWALE